OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI YA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI KWAKILOSA

S.L.P 842,

IRINGA.

KWA …….. (MWANAFUNZI)

K.K.…….(MZAZI/MLEZI)

YAH: MASHARTI YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KWAKILOSA

MWAKA 2021

Awali ya yote ninachukua nafasi hii kukupongeza kwa kufaulu mtihani wako wa darasa la saba, kitendo ambacho kinakuwezesha kuchaguliwa na kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule hii.

Shule ya sekondari kwakilosa ni shule ya kutwa na ni ya mchanganyiko. Umbali kutoka Irnga mjini hadi shuleni ni kilomita 08. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti na mzazi/mlezi wako shuleni kwa mashauriano ili kurahisisha ufanisi wa kazi yetu. Ninakutakia maandalizi mema kwa maagizo kama ifuatavyo:-

SARE YA SHULE

Wanafunzi wote wanatakiwa wawe na sare za kufanana ambazo zitashonwa mahali popote.

1. WASICHANA
   a) Sketi mbili za rangi ya kijani mpauko. Iwe ndefu kiasi cha kufunika soksi.
   b) Sweta moja ya rangi ya kijani.
   c) Mashati mawili ya mikono mifupi meupe
   d) Tai ya kijani mpauko (rangi ya sketi)
2. WAVULANA
   a) Suruali za rangi ya kijani mpauko. Zisiwe za kubana (modo)
   b) Sweta moja ya rangi ya kijani
   c) Mashati mawili ya mikono mifupi meupe.
   d) Tai ya kijani mpauko (rangi ya suruali)

MAHITAJI MENGINE

1. a) jozi mbili za viatu vya ngozi vyeusi visivyo na kisigino kirefu na vinavyofungwa kwa kamba.
   b) jozi mbili za soksi nyeupe kwa wasichana na wavulana.
   c) nguo na viatu vya michezo vitakavyovaliwa siku za michezo tu ambavyo ni raba nyeupe na trucksuit nyekundu za kitambaa laini na mistari miwili myeupe.

2.a) Pia aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa na faili.

b) Aje na picha 4 za rangi akiwa amevaa blauzi au shati nyeupe (PPS).

c) Daftari (counter books) Quire 2 na Quire 3 ziwe 10. Mkebe, kalamu na penseli, begi la kubebea vifaa vya shule. Mzazi /mlezi pia utagharamia

3. a) Kulipia nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani.

b) kugharimia matibabu ya mwanafunzi pindi auguapo.

c) RIMU (Bunda moja la karatasi) A4-80G kwa mwaka mzima.

d) Jembe moja na mpini wake.

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI YA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI KWAKILOSA

S.L.P 842,

IRINGA.

Sheria za shule ni hizi zifuatazo:-

1. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia vileo vyovyote kama pombe, madawa ya kulevya, bangi, kubeli n.k Mwanafunzi akibainika na kosa hili atafukuzwa shule maramoja.
2. Kila mwanafunzi atatakiwa kuwa mwaminifu kwa kuhudhuria vipindi vyoye vya shule bila kukosa labda kwa sababu maalum za kimsingi. Lakini taarifa itolewe na mzazi au mlezi shuleni.
3. Kila mwanafunzi atatakiwa kuwa mwaminifu, mtii kwa walimu na wafanyakazi wote wa shule.
4. Mwanafunzi hatakiwi kutoka nje ya mipaka ya shule au eneo la shule bila ruhusa maalum kutoka kwa mwalimu wa shule hii. Mwanafunzi atapewa kibali maalum kutoka kwa mwalimu wa zamu kwasababu maalum alizonazo nmwanafunzi.
5. Kila mwanafunzi lazima aheshimu kazi za mikono kama vileanavyopaswa kuheshimu masomo yake.
6. Kila mwanafunzi lazima aheshimu na kutunza mali za shule kwa ujumla wake. Ni kosa kubwa kuharibu mali za shule kwa makusudi au uzembe. Hivyo kinacho haribiwa au kupotezwa hakuna budi kilipwe na muhusika.
7. Mwanafunzi haruhusiwi kufuga kucha , ndevu, kupaka rangi kwenye kucha au mdomo, kunyoa nyusi na kuvaa mavazi yasiyo na heshima.
8. Wanafunzi hawaruhusiwi kuwa na nywele ndefu, wala zenye dawa katika hali ya usafi, ikiwa pamoja na kunyoa mitindo isiyokubalika.
9. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia Lugha ya matusi, maneno ya kashfa na kupigana, kosa la kupigana mwanafunzi atafukuzwa shule.
10. Urafiki wa kimapenzi kati ya wavulana na wasichana hauruhusiwi kabisa. Kosa hili ni sawa na mwanafunzi kupata mimba, kusababisha mimba au kutoa mimba na kushiriki kutoa mimba. Adhabu ya makosa haya ni kufukuzwa shule mara moja.
11. Ni marufuku kwa mwanfunzi kuwa na muziki (radio), simu za mkononi, kamera au vifaa vingine vya muziki ikiwa ni pamoja na flash, CD au Memory card n.k
12. Kuchelewa kufika shule asubuhi ni kosa
13. Tabia njema ukiwa shuleni na nje ya shule ni wajibu wa kila mwanafunzi wa shule hii.
14. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda nyumbani kwa mwalimu wake bila sababu maalum. Mwanafunzi akibainika atachukuliwa sheria za kinindhamu.
15. Ni marufuku kwa wanafunzi kuwepo katika nyumba za wageni (guest house), kumbi za starehe, vilabu vya pombe, bar n.k. Adhabu ya makosa haya ni kufukuzwa shule mara mwanafunzi akibainika na makosa haya.

SHERIA ZA MADARASANI

1. Kelele za darasani zinakatazwa, ukibainika unafanya hivyo adhabu yake ni kali. Darasani ni mahali pa kujifunzia siyo kupiga kelele.
2. Kila mwanafunzi anatakiwa kukaa darasani kufuatana na mpango uliowekwa na uongozi wa shule.
3. Hakuna mwanafunzi anayeruhusiwa kuandika darasani.
4. Mwanafunzi haruhusiwi kuandika au kuchora michoro kwenye ukuta au mbao za shule hii. Atakayebainika ataadhibiwa kisheria.

ADHABU

1. Mwanafunzi yeyote akipewa adhabu na mwalimu ni lazima aifanye kinyume chake atasababisha matatizo mengine
2. Makosa makubwa yataadhibiwa na mkuu wa shule au kwa kibali chake.

Ahsante

DARIO GAKALA

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI KWAKILOSA

MANISPAA YA IRINGA.

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI YA MITAA

HALMASJHAURI YA MANISPAA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI KWAKILOSA

S.L.P 842,

IRINGA.

A. YAH: MWANAFUNZI KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YA KUJIUNGA

Mimi …… nimesoma kwa makini barua na masharti ya kujiunga pamoja na sheria/ kanuni za shule ya sekondari Kwakilosa kwa heshima na unyenyekevu ninakubali/ninakataa nafasi hiyo kwa sababu……

Ninayakubali/ ninayakataa masharti/ sheria za shule kwasababu.

B. YAH: MZAZI/MLEZI KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YA KUJIUNGA

Mimi ……mzazi/mlezi wa …… ambaye amechagauliwa shule ya sekondari Kwakilosa nimesoma masharti ya kujiunga pamoja na sheria ya kujiunga na shule hiyo katika muda uliopangwa.

Ahsante

Jina la mzazi/Mlezi ……..

Anuani ……

Kitongoji/ Mtaa ninaoishi ……

Namba ya simu ya nyumbani …….

Saini……. Tarehe ……

Mzazi/mlezi akibadilisha anuani au kuhama, atujulishe mara moja anuani mpya.

C. MAMBO YA KUZINGATIA

i. Kumbuka kwamba mwanafunzi awe ameripoti shuleni si zaidi ya siku 21 baada ya shule kufunguliwa.
ii. Mwanafunzi anaposhindwa kufika shuleni kutokana na ugonjwa au tatizo lolote, mzazi/mlezi afike shuleni kutoa taarifa kwa mkuu wa shule siku hiyohiyovinginevyo atahesabiwa mtoro. Ruhusa kwa njia ya simu hazikubalwi
iii. Kila siku mwanafunzi akisharipoti shuleni haruhusiwi kuondoka bila ruhusa maalum ya mwalimu na atapewa kibali
iv. Mwanafunzi asipofika shuleni kwa muda wa siku 5 atasimamishwa shule.
v. Ni matumaini ya uongozi wa shule kwamba mzazi/mlezi atakuwa karibu na mwalimu katika kufuatilia mahudhurio, maendeleo, tabia na mwenendo wa mwanafunzi
vi. Iwapo mzazi/ mlezi atabadili anuani ni muhimu mzazi/mlezi mwenyewe aijulishe shule kwa kuambatanisha uthibitisho maalum ili iwe rahisikufanya mawasiliano. Aidha iwapo mwanafunzi atalazimika kuhama shule, lazima mzazi/mlezi (siyo mwanafunzi) atoe maelezo yenye kuthibitisha sababu za uhamisho huo.
vii. Kila mwanafunzi awapo shuleni ahudhurie vipindi vyote. Mwanafunzi akikosa vipindi 10 (asilimia 7 ya vipindi) kwa mwezi bila sababu zinazokubalika atarudishwa nyumbani.

IFAHAMIKE WAZI KUWA MAENDELEO YA WANAFUNZI YANATEGEMEA ZAIDI BIDII NA NIDHAMU YA MWANAFUNZI KWA HIYO TUNAHITAJI SANA USHIRIKIANO KWAKO MZAZI/MLEZI/MWANAFUNZI ILI KULETA UFANISI

KARIBU SANA KATIKA BSHULE YA SEKONDARI KWAKILOSA

NINAKUTAKIA MAFANIKIO MEMA KATIKA MASOMO

……

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI KWAKILOSA

MANISPAA YA IRINGA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI YA MITAA

HALMASJHAURI YA MANISPAA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI KWAKILOSA

S.L.P 842,

IRINGA.

DAKTARI ……

HOSPITALI YA ……

S.L.P ……..

YAH: FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI

Tafadhali tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu kwa gharama za mzazi/mlezi wake na athibitishwe kama ataweza kumudu masomo ya sekondari katika shule hii

Ni muhimu apimwe kabla hajaripoti ili kujua afya yake.

…….

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI KWAKILOSA

MANISPAA YA IRINGA.

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI KWAKILOSA

MWANAFUNZI ……

Aina ya vipimo vya mwanafunzi aliyetajwa hapo juu ni kama ifuatavyo:-

1. Urine
   …….
2. Stool
   ……
3. HB
   ……
   …
4. Pregnancy test ……..
5. Spleen
   ……..
6. Chest
   …….
7. Eyes
   ……
8. Ears
   ……..
9. Physically abnormality …….
10. Maelezo mengine…….

Nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu …….. taweza kumudu masomo ya sekondari

…… …… …… ……

JINA LA DAKTARI CHEO SAHIHI TAREHE